



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MEATU**



Meatu  
18 Julai 2022

**TANGAZO KUHUSU MAOMBI YA MIKOPO YA ASILIMIA KUMI (10%) YA  
MAKUSANYO YA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu anavitangazia Vikundi vya Wanawake, Vijana, na Wenye Ulemavu kuomba mikopo inayotokana na asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Masharti na Vigezo Vinavyotakiwa:

- i. Hati ya Usajili (usajili huo unafanyika kwa njia ya Mtandao, kwa maelezo zaidi fika Ofisi ya Maendeleo ya Jamii)
- ii. Katiba ya kikundi iliyosainiwa na Mwanasheria/Hakimu/Wakili
- iii. Kikundi kiwe na Akaunti Benki
- iv. Kikundi kiwe na mradi au wazo la kuanzisha mradi unaopimika
- v. Andiko fupi la mradi (Mchanganuo wa Mradi)
- vi. Kikundi kiwe kinatambulika kuanzia ngazi ya Kijiji hadi Kata
- vii. Kisiwe na deni katika taasisi yoyote
- viii. Ni lazima kila Mwanakikundi awe na Kitambulisho cha Taifa au Namba (NIDA)
- ix. Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, S.L.P 44, Kupitia Kwa Mtendaji wa Kata na Kijiji

*Ikumbukwe kuwa vikundi vyenye miradi ya kuongeza thamani kwenye bidhaa za kilimo, mifugo, misitu na maliasili (mfano uchakataji wa zao la alizeti, pamba, asali, ngozi, maziwa, useremala na ucholemeaji) vinahamasishwa kuomba mikopo.*

  
Benton Nollo

Mkuu wa Kitengo cha Mawasilano Serikalini, Meatu



**Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne Tarehe 23 Agosti 2022**